# TANROADS

Jarida Maalumu Novemba 2022

Tanzania National Roads Agency TANROADS Good roads for national development


# Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea na ukarabati na Ujenzi wa Viwanja vya Ndege

"Hii ni dhamira kubwa iliyokuwa nayo serikali ya awamu ya sita kuhakikisha sekta ya anga inakuwa na hakuna kitakachokwamishwa Tumekuwa na falsafa yetu ya kukuza ushirikiano kwa ajili ya maendeleo..."

Rais Samia



Limeandaliwa na kitengo cha Habari na Mawasiliano- TANROADS

# Serikali ya Awamu ya Sita itaendelea na ukarabati na Ujenzi wa Viwanja vya Ndege



**NA LELA MUHAJI, DODOMA.**

RAIS wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amesema serikali ya awamu ya sita itaendelea kukarabati na kujenga viwanja vya ndege nchini ili kuweza kukuza sekta ya usafiri wa anga na kuchochea uchumi wa nchi.

Akizungumza, katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Rais Samia amesema kiwanja hicho kitakapokamilika kitabadilisha taswira ya mkoa wa Dodoma, ambao sasa ni makao makuu ya nchi, huku akisisitiza azma na maono ya serikali ya kujenga kiwanja hicho sasa inakwenda kutimia na kusisitiza kuwa kitarahisisha usafiri wa anga kutoka mkoa wa Dodoma na mikoa mingine pamoja na usafiri wa ndege wa kimataifa.

Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato kinajengwa kwa ushirikiano wa Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) kwa gharama ya dola milioni 329.64 ukiwa ni mkopo wenye masharti nafuu.

"Kazi ya kukuza na kuendeleza usafiri na usafirishaji wa anga unaendelea kwa kasi kubwa na malengo ya serikali ni kujenga viwanja vya ndege katika kila mkoa" alisema Mhe. Rais.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali inakarabati na kujenga viwanja mbalimbali vya ndege katika mikoa ya Shinyanga, Mtwara, Iringa, Musoma, Songea na Songwe ambapo muda wowote kuanzia sasa ujenzi wake unakaribia kukamilika.

"Hii ni dhamira kubwa iliyokuwa nayo serikali ya awamu ya sita kuhakikisha sekta ya anga inakuwa na hakuna kitakachokwamishwa. Tumekuwa na falsafa yetu ya kukuza ushirikiano kwa ajili ya maendeleo" alisema.

Rais Samia aliipongeza AfDB kwa ushirikiano waliotoa pamoja na wadau wengine wa Maendeleo ikiwemo BADEA, OPEC ambao walianza mchakato mapema ya usanifu wa kiwanja, ambapo sasa Benki ya Maendeleo ya Afrika imetoa mkopo wa ujenzi wake.

Mhe Rais, alisema ana matumaini makubwa kuwa ujenzi wa kiwanja hicho kitakamilika kama ilivyopangwa Desemba 2024 ili huduma zianze kutolewa katika kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato.

Kwa upande wake, Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Profesa Makame Mbarawa alimpongeza Rais Samia kwa juhudi kubwa aliyokuwa nayo katika sekta ya ujenzi.

Alisema ujenzi wa kiwanja hicho umetekeleza nia ya serikali iliyokuwa nayo tangu mwaka 1970 ya ujenzi wa kiwanja hicho na kuanza kutafuta fedha kwa wadau mbalimbali wa maendeleo.

"Tutawasimamia Wakandarasi wote wanaotekeleza mradi huu ili uweze kumalizika kwa wakati na azma ya serikali ya kuboresha



viwanja vya ndege nchini itimie kwa nguvu kubwa" alisema.

Naye, Mwakilishi wa AfDB nchini Tanzania, Dk. Patricia Lavley alisema ujenzi wa kiwanja hicho ni fursa adhimu ya kukuza uchumi kupitia sekta ya anga na ana matumaini makubwa ifikapo 2024 kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato kitakamilika.

Kwa upande wake, Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Barabara Tanzania (TANROADS) Eng. Rogatus Mativila alisema, kiwanja cha bndege cha Kimataifa cha Msalato kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa kama 'Airbus'yenye uwezo wa kubeba abiria 500 na kitakuwa na njia mbli za kutua na kurukia ndege zenye upana wa mita 75 na urefu wa mita 4,500, Alisema.

Pia, alisema kutakuwa na majengo ya maalumu ya viongozi , kuhifadhi mizigo, watu mashuhuri, na jengo la kuhifadhi vifaa na mitambo ya kuhudumia ndege.

'Kutakuwa na jengo la watu mashuhuri, jengo lahuduma za kuzima moto, jengo la kuhifadhia mitambo ya kuruka ndege, jengo la maegesho na uwekezaji wa kiuchumi.' Alisema.

Aidha, Mtendaji Mkuu alisema kutokana na usanifu uliofanyika mradi wa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha kimataifa cha Msalato utatekelezwa kwa awamu na kwenye awamu ya kwanza, utajengwa kwa daraja la 4E.

Kwa mujibu wa Eng. Mativila kiwanja hicho kinachojengwa na wakandarasi wawili kwa awamu ya kwanza kitagharimu dola milioni 329.64 ikiwa ni mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, unatarajiwa kukamilika Desemba, 2024






# Tanroads yajivunia mafanikio Ujenzi wa Barabara, Madaraja na Viwanja vya Ndege Nchini

Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng Rogatus Mativila amesema Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya utekelezaji wa majukumu ya TANROADS na vipaumbele kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Eng. Mativila ameyasema hayo katika mkutano na waandishi wa habari Jijini Dodoma wakati wa kuelezea mafanikio hayo ambapo amesema TANROADS imekuwa mstari wa mbele katika usimamizi wa miradi mbalimbali ya miundombinu ya ujenzi wa barabara, madaraja na viwanja vya ndege.

Amesema TANROADS ilianzishwa kwa Waraka wa Serikali uliotolewa katika gazeti la Serikali Na. 293 la tarehe 25 Agosti, 2000 kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997.

Lengo la kuanzisha kwa Wakala ni kuleta ufanisi zaidi katika majukumu yaliyokuwa chini ya Idara ya Barabara katika Wizara ya Ujenzi.

Wakala ulianza kufanya kazi rasmi tarehe 1 Julai, 2000 na hivyo nimeifikisha zaidi ya miaka 22 tangu kuanzishwa kwake" amesema.

Mhandisi Mativila amesema tangu kuanzishwa kwa TANROADS imeweza kusimamia majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo kuratibu , kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kuu na za Mikoa zenye urefu wa kilometa 36,362.

Alifafanua " TANROADS imekuwa na mipango mingi ili kuhakikisha nchi inakuwa na barabara nyingi za lami ikiwemo kushirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami"

Alitaja jukumu lingine la TANROADS ni kupima na kufanya utafiti kuhusu vifaa vya ujenzi wa barabara kupitia Kitengo cha Maabara Kuu ya Vifaa ( Central Materials Laboratory) na maabaa ndogo zilizopo katika kila mkoa.

Aidha, alisema kumekuwa na mafanikio makubwa ya ujenzi wa madaraja na viwanja vya ndege chini ya uongozi wa Rais Samia kwakuwa amekuwa mstari wa mbele kwa kutoa fedha kwa wakati na maelekezo bora yaliyokuwa na ufanisi kwao.





# MATUKIO MATIKA PICHA

## HAFLA YA UWEKAJI JIWE LA MSINGI LA MRADI WA UJENZI WA KIWANJA CHA NDEGE CHA KIMATAIFA CHA MSALATO, JIJINI DODMA OKTOBA 30, 2022.










*Tangu kuanzishwa kwa TANROADS imeweza kusimamia majukumu yake kwa ufanisi mkubwa ikiwemo kuratibu , kusimamia ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara kuu na za Mikoa zenye urefu wa kilometa 36,362.*

***Mtendaji Mkuu wa TANROADS Eng Rogatus Mativila***




**TANROADS**
Makao Makuu Ghorofa ya 3, 10
Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue
S.L.P 11364 Dar es Salaam
Baruapepe: Tanroadshq@tanroads.go.tz

***" Miundombinu bora ya barabara, madaraja na viwanja vya ndege kwa maendeleo ya Taifa"***